**Mitazamo ya Familia za Kaunti ya Hillsborough kuhusu Ufadhili wa Shule**

Maoni ya familia ni muhimu kuhakikisha kuwa bajeti za shule zinalingana na mahitaji ya jamii na vipaumbele vya wanafunzi wetu. Chunguza nyenzo hii ili upate maelezo zaidi kuhusu ufadhili wa shule, ikiwa ni pamoja na vipaumbele vya familia kuhusu matumizi. Shiriki maelezo haya katika jamii yako na utumie matokeo haya kutetea mabadiliko unayotaka yafanyike.

Changamoto iliyosababishwa na mizuko mingi ya mwaka wa shule wa 2020-21 imetatiza hatua za kushirikisha familia kwa kina na kufadhili unafuu na urejesho unaohitajika ili kuwawezesha wanafunzi kusoma na kustawi. Mwaka huu, Chama cha Walimu na Wazazi cha Halmashauri ya Kaunti ya Hillsborough kilishirikiana na Chama cha Walimu na Wazazi cha Kitaifa kama sehemu ya mpango wa kusikiliza kwa makini – na kujibu – maswali na wasiwasi wa wanafamilia kuhusu ufadhili wa shule. Wanafamilia wanajua nini kuhusu ufadhili wa shule katika Shule za Kaunti ya Hillsborough? Wanafamilia wanahisi ni vipengele gani vilivyofadhiliwa vya kutosha au visivyo vya kutosha? Wanafamilia wana maoni gani kuhusu tofauti za ufadhili wa kila mwanafunzi katika jamii?

Hasa, Chama cha Walimu na Wazazi cha Halmashauri ya Kaunti ya Hillsborough kilisaidia kufanya vikao vya kusikiliza maoni ya wanafamilia na kusambaza tafiti kwa familia ili kufumbua vipaumbele vya jamii na kuchangia katika utafiti wa kitaifa kuhusu ufadhili wa elimu. Washiriki 34 walihudhuria vikao vya kusikiliza vya mtandaoni vinavyowezeshwa na wafanyakazi wa Chama cha Walimu na Wazazi cha Kitaifa. Tazama Kiambatisho cha A uone jedwali la demografia ya wazazi wanaoshiriki.

## Mafunzo Makuu

1. **Wanafamilia wanahisi kuwa hawafahamu bajeti za shule na hawana uhakika wanapaswa kwenda wapi kupata maelezo.** Ni asilimia 32 tu ya washiriki wa Kaunti ya Hillsborough walikubali kuwa wana uelewa wa jumla kuhusu jinsi wilaya ya shule ya watoto wao inatumia ufadhili inayopokea, na ni asilimia 27 tu waliokubali kuwa walijua mahali pa kupata maelezo kuhusu ufadhili wa shule katika jamii yao.

   > *"Kwa kweli sijui sana ufadhili wa shule hutoka wapi. Pengine ushuru wa mali na vitu kama hivyo."*

2. **Wanafamilia wanathamini usawa wa elimu na hupendelea shule zipokee fedha kulingana na mahitaji.** Asilimia 79 ya washiriki walisema kuwa wanaamini shule zinapaswa kupata ufadhili kulingana na mahitaji, ikilinganishwa na asilimia 30 ambao walisema kuwa waliamini shule zinapaswa kupokea kiasi sawa cha ufadhili.

   > *"Ningependa shule za Kiwango cha 1 au za Mwamko zipewe ufadhili zaidi. Nadhani hatua hii inahitajika, kwa sababu hazina familia zilizo na mapato ambayo yanaweza*

3. **Gharama zinazohusiana na shughuli za msingi za shule hulipwa kwa usaidizi wa Chama cha Wazazi na Walimu na/au juhudi zingine za kuchangisha fedha.** Washiriki walibaini kuwa Vyama vyao vya Wazazi na Walimu vilifanya ufadhili kutimiza mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya ofisi ya muuguzi shuleni, vifaa vya kiteknolojia na nyenzo za mtandaoni, na vifaa vingine vya shule.

> *"Sidhani kuna vifaa vya kutosha kwa sababu sisi kama Chama cha Wazazi na Walimu tunawapa walimu vifaa hivi, na wakati huu wa COVID wazazi wote walishirikiana kuwasaidia walimu kwa kuwapa vifaa. Tuliandaa mpango wa*

4. **Familia zinaamini kuwa shule zinahitaji ufadhili zaidi na zilitambua Walimu na Wasaidizi wa Walimu**, **Kufunza, Mipango ya Likizo na Baada ya Shule**, na**Washauri na Huduma za Ushauri kama vipaumbele.** Karibu nusu (asilimia 53) ya washiriki wanaamini shule ya watoto wao haipokei ufadhili wa kutosha. Pia, familia zilibaini vipaumbele vya kutoa ufadhili zaidi kwa:

   - ***Walimu na Wasaidizi wa Walimu***. Asilimia 53 ya washiriki walichagua Walimu na Wasaidizi wa Walimu kama mojawapo ya vipaumbele vyao vikuu vinavyohitaji ufadhili zaidi. Washiriki waliripoti kuwa wilaya inahitaji kuwaajiri walimu na wasaidizi wa walimu wengi zaidi, hasa ili kukabiliana na changamoto zilizosababishwa na COVID-19.

     > *"Binti yangu anashiriki katika IEP, na hivi sasa hawezi kupata masomo ya ziada ambayo anahitaji, kwa sababu hawana walimu wa kutosha."*
     >
     > *"Katika shule za upili, [kuna] masomo fulani hayafanyi kwa sababu ya uhaba wa walimu kufuatia janga hili."*

   - ***Kufunza, Mipango ya Likizo na Baada ya Shule*****.** Asilimia 50 ya washiriki walichagua Kufunza, Mipango ya Likizo na Baada ya Shule kama mojawapo ya vipaumbele vyao vikuu vinavyohitaji ufadhili zaidi. Ingawa washiriki hawakutoa maoni hasa kuhusu mipango hii ya baada ya shule, walisema kuwa kuwa kuna **haja ya shughuli zaidi zisizo za kielimu** ikiwa ni pamoja na muziki, sanaa na shughuli za michezo ambazo mara nyingi hupatikana katika mazingira haya. Hasa, **wazazi waligundua kuwa shughuli zisizo za kielimu, kama vile muziki, zilikuwa za gharama ghali.**

     > *“Kushiriki katika mpango wa muziki huwa na gharama kubwa. Ikiwa watoto wangependa kujiunga lakini wazazi wao hawawezi kumudu gharama au mpango wa ufadhili haujachangisha pesa za kutosha, basi mtoto huyo hawezi kushiriki.”*
     >
     > *"Binti yangu alikuwa akicheza tarumbeta, ambayo bei yake inaanzia dola elfu 10. Alikuwa akicheza tarumbeta iliyokuwa imevunjika. Hatuwezi kupata fedha za kutosha za kununua vyombo hivi vyote, lakini sidhani*

- ***Huduma za Ushauri*.** Asilimia 47 ya washiriki walichagua Huduma za Ushauri kama mojawapo ya vipaumbele vyao vikuu vinavyohitaji ufadhili zaidi. Washiriki walisema kuwa kulikuwa na haja ya kuwaajiri washauri zaidi. Washiriki walisema kuna ukosefu wa huduma zinazopatikana, haswa kwa wanafunzi wa mtandaoni, na muda mrefu wa kusubiri miadi.

*"Nadhani kweli tunahitaji washauri zaidi, wanasaikolojia na wahudumu wa kijamii katika shule hizo. Kuna mhudumu mmoja wa kijamii kwa watoto 2,000, na kuna mwanasaikolojia mmoja kwa watoto 2,000, na idadi hiyo haitoshi hata kidogo."*

*"Hakujawahi kuwa na washauri na wanasaikolojia wa kutosha katika shule yoyote niliyohudhuria. Ukirudi kwenye daraja la kwanza wakati watoto walipaswa kupimwa kwa*

- **Katika vikao vya usikilizaji, wafamilia pia waliangazia maswala yanayohusiana na ukosefu wa fedha kwa huduma maalum.** Hoja za mara kwa mara zilijumuisha ukosefu wa msaada wa kibinafsi na vifaa muhimu. Washiriki pia walisema kuwa kuna haja ya kutoa usaidizi zaidi kwa wanafunzi wa lugha ya Kiingereza na familia zinazozungumza lugha mbili, hasa wakati wa janga hili.
- **Ikiwa watalazimika kupunguza matumizi, wanafamilia wa Hillsborough waligundua vipaumbele vifuatavyo** ambavyo matumizi yake yanapaswa kupunguzwa: **Majukumu ya Ofisi Kuu ya Wilaya** (79%), **Maafisa wa Usalama na Usaidizi wa Shule** (24%), **Muziki na Sanaa** (21%), **Nyenzo za Shule** (21%), **Huduma za Maktaba** (21%) na **Huduma kwa Wanafunzi wenye Talanta Maalum** (21%). Kumbuka: Ingawa Muziki na Sanaa ziliorodheshwa kuwa vipengele ambavyo gharama yake inaweza kupunguzwa, mazungumzo ya vipindi vya usikilizaji pia yalionyesha kuwa muziki na sanaa tayari zilikuwa hazina ufadhili wa kutosha.

## Hatua Ambazo Watetezi Wanaweza Kuchukua

***Fahamu maelezo kuhusu matumizi ya wilaya ya shule yako na ujaribu kugundua mitindo maalum.***

- Chanzo cha msingi cha ufadhili wa Shule za Kaunti ya Hillsborough ni mapato ya ndani (49%), yakifuatiwa na mapato ya serikali (40%) na shirikisho (11%).

- Asilimia 71 ya bajeti ya Shule za Kaunti ya Hillsborough hutumika kukidhi gharama za wafanyakazi (mishahara na marupurupu ya wafanyakazi)

- Wastani wa matumizi kwa mwanafunzi mmoja (PPE) katika Shule za Kaunti ya Hillsborough katika Mwaka wa Kifedha wa 2019 ulikuwa $8,973, kiasi ambacho kilikuwa chini sana kuliko wastani wa kitaifa wa $14,439.
- Shule za Hillsborough zilizo na matumizi ya juu zaidi kwa kila mwanafunzi ni:
    - Channelside Academy of Math & Science ($29,001)
    - Creekside Charter ($25,582)
    - Independence Academy ($24,092)
- Shule za Hillsborough zilizo na matumizi ya chini zaidi kwa kila mwanafunzi ni:
    - Florida Connections Academy ($5,316)
    - Southshore Charter ($5,766)
    - Winthrop Charter ($5,769)
- Elewa ni kwa nini matumizi yanaweza kutofautiana: mahitaji ya wanafunzi, mipango maalum, mgawanyo usio na usawa.
- Linganisha matumizi na matokeo. Baini ni mitindo gani inayoibuka!
- Unaweza kukusanya maelezo zaidi kila mwaka kwenye kadi ya ripoti ya serikali. Anzia hapa!

***Shiriki katika michakato ya mipango ya wilaya.***

- Elewa awamu za bajeti ya wilaya yako.
- Fahamu wakati bodi yako ya shule hukutana na uhudhurie au kutazama rekodi za video. Toa mawazo na ueleze wasiwasi wako wakati wa vipindi vya kutoa maoni vya umma.

***Waulize wanabodi wa bodi ya shule yako na maafisa wa wilaya maswali ili upate maelezo zaidi. Haya hapa maswali machache ya kukusaidia kuanza:***

- Ni sababu gani zinazosaidia kubaini matumizi kwa kila mwanafunzi kwa kila shule?
- Wilaya inaamuaje vipengele ambavyo watahitaji kufadhili kwa pesa zake?
- Ni njia gani bora kwa wanajamii kushiriki maoni yao kuhusu vipaumbele vya bajeti?

## Wasiliana Nasi

Wasiliana na Chama cha Wazazi na Walimu cha Kaunti ya Hillsborough kupitia president@hccptaptsa.org

Viambatisho

*Kiambatisho cha A – Maelezo ya Kidemografia ya Washiriki wa Hillsborough*

| Ukoo/Kabila | | | | | Mapato | | | Jinsia | | Elimu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mzungu au Mtu Mweupe | Mlatino au Mtu wa Asili ya Uhispania | Tabaka 2 au zaidi | Mwafrika Mmarekani au Mtu Mweusi | Mwesia au Mkazi wa Visiwa vya Pasifiki | Chini ya elfu $50 | Eldu $50-100 | Zaidi ya elfu $100 | Kike | Kiume | Cheti cha Shule ya Sekondari au zaidi | Shahada ya Chuo Kikuu au zaidi |
| 21% | 44% | 12% | 21% | 3% | 47% | 26% | 26% | 88% | 12% | 100% | 65% |